**LEARNING BY EAR 2012**

**"Bado ningali mwanadamu- Riwaya inayoangazia matatizo wanayopata watu wanaougua maradhi ya akili barani Afrika"**

**EPISODE 3: "Kutafuta jawabu"**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Pendo Paul**

**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**<u>SCENE ONE: MALEMBA NA CHUMBA WAFIKA PANGONI KWA MIZANJA</u>**

- **Malemba (mke, 35)**
- **Mizanja (mume, 65)**
- **Msimulizi**

**<u>SCENE TWO: VALERIE NA IRENE KATIKA KIHOTELI CHUONI</u>**

- **Valerie (mke, 19)**
- **Irene (mke, 19)**
- **Msimulizi**

**<u>SCENE THREE: VALERIE AENDA KUMTEMBELEA DKT. MAHIRO KATIKA HOSPITALI KUU</u>**

- **Valerie (mke, 19)**
- **Mahiro (mume, 50)**

**UTANGULIZI:**

Hujambo mpenzi msikilizaji na karibu katika kipindi che redio ukipendacho cha **Noa bongo, Jenga maisha yako**. Hiki ni kipindi cha tatu kinachoangazia masaibu ya watu wanaougua maradhi ya akili barani Afrika kwa jina, **“Bado ningali mwanadamu”.** Kipindi kilichotangulia, mwanafunzi wa uuguzi Valerie alianza kusikia sauti za watu wasioonekana. Haya yalimshtua rafiki yake Irene aliyekimbia kutafuta msaada, kule shuleni. Kwengineko, Malemba alifurumushwa na kijana wake Chumba aliyekuwa na homa kali, hii ni kwa sababu nesi Matilda hangelihudumia watu punguani. Na baada ya Kapaka kupoteza kazi yake dukani, mkewe Cheupe alimshangaa kwa kususia mazoezi ya kwaya, jambo ambalo hajawahi kulifanya hapo kabla. Ndiyo kwanza tunaona wagonjwa wa akili wakianza kutengwa na kuhujumiwa. Kipindi cha leo kinaitwa **“Kutafuta jawabu”.**

Ni jioni tulivu wakati ambapo Malemba amewasili na kijana wake Chumba pangoni kwa Mizanja.

**SCENE ONE: MALEMBA NA CHUMBA WAWASILI PANGONI KWA MIZANJA**

1. **ATMO: EVENING AMBIENCE IN THE VILLAGE**

2. **MIZANJA:** **(singing songs that can't be understood)**

3. **MALEMBA:** Habari za jioni, Mizanja, mganga wa waganguzi.

4. **MIZANJA:** Salama, Malemba. Nikusaidie nini wewe na kijana wako?

5. **MALEMBA:** Ana homa kali, mwili wake unachoma hasa. Pia kichwa kinamlipuka. Waweza kumpatia dawa?

6. **MIZANJA:** **(a little grumpy)** Lakini homa na joto ni maradhi ya hospitali, ama? Isitoshe saa hizi sishiki tena dawa.

7. **MALEMBA:** Unionavyo hivi, nimetoka huko hospitali, nesi akatuzuia tusimuone daktari. Asema Chumba ana wazimu kwa hivyo hospitali ile haina vifaa vya kumhudumia. Aliniambia Chumba anafaa kupelekwa jijini kwa matibabu maalum. Kwa ufupi, alitufukuza akisema ati Chumba anatishia wagonjwa wengine. Sina hata senti, haya huko mjini tutafikaje. Ndio maana unaniona hapa.

8. **MIZANJA:** **(thoughtful and more friendly)** Mmmh, sijui ni lini watu wenye maradhi haya ya akili watachukuliwa kuwa na hadhi sawa na wenye kuugua maradhi mengine. Si neno, nitakupa mizizi ukachemshe kisha maji yake umpe mwanao anywe leo usiku. Ametulia sana labda

maumivu yamekwisha.

9. **MALEMBA:** Usiku huwa mtulivu. Pepo humvamia mchana hasa wakati wa saa sita.

10. **MIZANJA:** Basi mlete mchana wakati mwengine nije niseme nao hao pepo watwambie kwanini wamechagua kumtesa mwanao. Kwa sasa chukua fungu hili la dawa na uende.

11. **SFX: SEVERAL LEAVES BEING PLUCKED FROM A PLANT**
**Or: Branch being ripped off a tree then handed over**

12. **MIZANJA:** Chemsha haya majani umpe Chumba anywe. Homa yote itapotea. Nenda na usiangalie nyuma. Nataka kuaga mababu na mizimu. **(starts to sing again)**

13. **MALEMBA:** Asante Mizanja. Nakushukuru sana. Twende Chumba, utapona mwanangu.

14. **MSIMULIZI:** Mara nyengine tena, Malemba na Chumba walianza safari. Malemba akiwa ameshika dawa mkono mmoja na mkono wa pili amemshika mwanae. Kweli Chumba atapona? Wacha tuone. Siku ya pili katika kihoteli pale chuoni, Valerie, cha ajabu amerudia hali yake ya kawaida na kumfanya rafikiye Irene asielewe kunaendelea nini.

**SCENE TWO: VALERIE NA IRENE KATIKA KIHOTELI CHUONI**

15. **ATMO:** **COLLEGE CANTEEN AMBIENCE**

16. **VALERIE:** Ni nini Irene? Mbona waniangalia kama ambae nimeshuka kutoka angani?

17. **IRENE:** Uhm… pole, Valerie. Sina la kusema baada ya kunitishia jana ati unasikia sauti za watu. Na nilipokimbilia usaidizi na kurudi baadaye, ulikuwa umeketi tuli kama vile hakuna kilichotokea...mimi nikaonekana mjinga.

18. **VALERIE:** Kwa sababu hakuna kilichotokea! Labda nilikuwa najiongelesha na wewe ukafikiri nina wazimu **(laughs).** Masikini pole, sasa wewe ndiyo ukaonekana mwenda wazimu.

**IRENE:** Sawa lakini Valerie ukifanya tena hivyo itabidi mimi nihamie chumba kingine sipendi matani kama hayo**.**

19. **VALERIE:** **(laughs softly)** Mmh.. usijali niko sawa.

20. **IRENE:** Nisubiri naenda msalani naja….

21. **VALERIE:** Hata mimi nilikuwa nimebanwa, twende sote.

**(They both laugh and stand up)**

22. **MSIMULIZI:** Irene anafikiria Valerie amepona hivi sasa. Lakini punde si punde atafahamu hamjui vizuri swahiba wake. Watakapoingia msalani tu, kizaazaa kitazuka tena..

23. **SFX:** **TOILET BEING FLUSHED**

24. **SFX:** **TOILET DOOR OPENING**

25. **IRENE:** Valerie! He, chakula chetu kinapoa. Tuoshe mikono mara moja turudi. Mbona wajiangalia sana kwenye kioo? Hujiamini u mrembo?

26. **VALERIE:** **(mumbling words)** Unamtazama nani?

27. **IRENE:** Ati namtazama nani? Wewe bila shaka!

28. **VALERIE:** **(louder, as if to somebody else)** Wacha! Wazungumza na nani? Sitaki kusikia sauti yako!

29. **IRENE:** Acha zihaka Val! Kwanini hutaki kusikia sauti yangu? Ah, Valerie! Twende nafasi zetu zitachukuliwa tumekawia sana, eti.

30. **VALERIE:** **(interrupts, shouting)** Usinitazame! Husikii! Sitaki uniongeleshe **(angry)** Ntakupiga!

31. **SFX:** **MIRROR BREAKING INTO PIECES AS SHE HITS IT WITH HER FIST**

32. **VALERIE:** **(screaming in pain)** Aaaah!

33. **IRENE:** Valerie, umejikata mwenyewe? Kwanini ufanye hivyo?

34. **VALERIE:** Irene, nini kimetokea? Mbona ninatoka damu kwenye mkono wangu?

35. **IRENE:** Ni mimi ninafaa kukuuliza wewe sawali hilo…. Lakini kwanza hebu nikufunge ili damu isitoke zaidi.

36. **SFX:** **ZIPPER OPENING, SEARCHING IN HER BAG**

37. **IRENE:** Hebu nikufunge, usipoteze damu nyingi zaidi.

38. **SFX**: **HANDKERCHIEF BEING WRAPPED AROUND HAND**

39. **IRENE:** Kwani una nini. Mara unasema na mimi na mara unapiga mayowe kwenye kioo. Valerie, hii si mara ya kwanza kunishtua, kwanini usimuone mtaalam wa akili dadangu...

40. **VALERIE:** **(crying)** Sijui nina shida gani, siwezi kujizuia.

41. **MSIMULIZI:** Irene anasema kweli. Valerie anafaa kutafuta jibu la tatizo lake. Tabia zake zimeanza kuwa hatari sasa. Kwa bahati, mtaalamu hayuko mbali kwa hivyo, baada ya lishe Valerie alikwenda kumuona Dkt. Mahiro. Mtaalam pekee nchini anayehudumia takriban watu milioni 5. Endelea kusikiliza.

**<u>SCENE THREE: VALERIE AKUTANA NA DKT. MAHIRO KATIKA HOSPITALI KUU</u>**

42. **ATMO:** **HOSPITAL AMBIENCE INSIDE DOCTOR’S ROOM**

43. **MAHIRO:** **(calls out)** Mwengine!

44. **SFX:** **DOOR SLOWLY BEING OPENED**

45. **MAHIRO:** Naam, Binti, nikusaidieje… Keti unieleze: Nikusaidieje?

46. **VALERIE:** **(embarrassed)** Nianzie wapi…um… naitwa Valerie. Rafiki yangu Irene anasema mimi akili yangu haiko sawa, kwa hivyo ili iwe sawa ni muhimu nikuone wewe daktari kwa sababu daktari mtaalamu ni wewe peke yako....

47. **MAHIRO:** Sawa. Vyema. Rafiki yako anasema wewe una tatizo la akili, na je wewe mwenyewe unahisi vipi?

48. **VALERIE:** Sijui, mimi naona niko sawa.

49. **MAHIRO:** Mimi nina uzoefu wa kazi hii. Wengi wa watu hufikiri kuwa hawana wazimu ilhali vitendo vyao hata vinazidi wenye kuugua akili. Turudie mjadala wetu. Unajifunza uuguzi?

50. **VALERIE:** **(shocked)** Naam! Ndiyo! Umejuaje? Unaweza kuisoma akili yangu pia?

51. **MAHIRO:** **(laughs heartily)** Hahaha…bila shaka kama mtaalam wa akili lazima niweze kusoma akili yako! Nakutania... nimeona sare uliyovaa na jinsi ulivyofungwa mkono wako bila shaka umefungwa vizuri na mwanafunzi mwenzako sivyo? Mkono umefanywaje? Au umejikata kwa wembe?

52. **VALERIE:** La daktari. Hapo ndio utata ulipoanzia. Ila nafikiri nilijiumiza mwenyewe. Irene, rafiki yangu anasema ati nilipoingia msalani na kuona kioo basi nilianza kuongea peke yangu na kioo. Kisha nikavunja kioo kwa kukipiga ngumi ndio kikanikata.

53. **MAHIRO:** Unajua ni kwanini ulifanya hivyo?

54. **VALERIE:** Irene alisema nilikuwa naongea peke yangu na sauti ambazo yeye alikuwa hazisikii... kwani nimepatwa na nini?

55. **MAHIRO:** Valerie, nahitaji tuwe tukionana mara kwa mara ili nijue fika tatizo lako ni nini. Nahisi japo sina hakika kuwa una tatizo la akili.

56. **VALERIE:** **(shocked)** Ati tatizo la akili?

57. **MAHIRO:** Usiogope, hata nami nashuku tu kwa sasa. Isitoshe tuna uhaba wa maabara yanayofana utafiti wa maradhi mengi ya akili na maradhi haya huchukua muda mrefu kujulikana. Hata hivyo, tukionana nitazidi kukuelewa unachopitia... hata hivyo, matibabu na ufuatiliaji mzuri ukiwepo mtu hupona na kurudia hali yake ya kawaida.

58. **VALERIE:** Asante daktari. Wewe unafikiria mimi naweza kuwa nina wazimu?

59. **MAHIRO:** Hapana. Wewe ni mgonjwa wangu na kamwe siwaiti wagonjwa wangu wendawazimu.

**OUTRO:**

Kwa uhakikisho huo kutoka kwa Dkt. Mahiro, tunafunga kipindi chetu cha tatu kwa jina, **“Bado ningali mwanadamu”**. Hadithi inayoangazia masaibu ya watu wanaoagua maradhi ya akili barani Afrika. Je, Dkt. Mahiro atamsaidia Valerie? Chumba atapona na kufuata maisha yake ya kawaida? Hatima ya Kapaka ni ipi kutokana na hali yake hii mpya? Patiliza yote hayo na mengineyo katika kipindi kifuatacho. Kusikiliza tena kipindi hiki au chengine kilichopita mwanzoni tembelea tovuti yetu dw.de/lbe. Mpaka tutakapoonana tena, kwa heri.